
TAWLA


## Chama Cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA)


# Zijue kanuni na Taratibu za sheria Katika masuala ya ardhi na jinsia


Sida


WE EFFECT


Je kama mtu ameniibia hati miliki yangu ya kimila halafu amekwenda kuuza shamba langu, Ni taratibu gani ninaotakiwa kufanya ili kupata hati yangu?
Unachotakiwa kufanya upotezapo hati miliki yako ni kutoa taarifa ya kuibiwa au kupotelewa kwa hati, taarifa hii hutolewa polisi. Kama imeibiwa utafungua mashtaka ya wizi pia. Mashtaka hayo utafungua dhidi ya aliyeuza na aliyenunua ardhi yako, mahakama ikijiridhisha kuwa ardhi inayobishaniwa pamoja na hati ni vyako, itaamuru urudishiwe ardhi pamoja na hati yako.


Je, ni nani muhusika wa kulipa fidia pindi ardhi inapotwaliwa na mgeni au serikali kwa shughuli za uwekezaji?
umeuliza swali zuri sana
Kwa kuwa suala la fidia huja baada ya mchakato wa makubaliano ya uwekezaji au utwaaji wa ardhi baina ya mwekezaji au Rais na Wanakijiji, basi wakati taarifa za utwaaji au uhawilishwaji ardhi zinawafikia wanakijiji watakuwa na nafasi ya kuuliza na kujua ni nani atawalipa fidia


Hehee!! jamani ule wakati ambao tulikuwa tukiungojea umekaribia, tujiandae.. Mkutano mkuu wa kijiji unakaribia, tujiandae kupeleka ajenda zetu ili zijadiliwe na sheria zitungwe tuishi kwa kuheshimiana na kupeana haki sawa.
Kwani mkutano mkuu wa kijijii unatakiwa kuongelea mambo gani? unajua wanaume huwa hawamalizi kubishania mambo yao. Je, ya kwetu yataingia wapi?
Mimi nilipata nafasi ya kuhudhuria semina kuhusu mambo ya urasimishaji ardhi. Pia nilianza kuulizia kwa wasaidizi wa sheria na viongozi wa kijiji na hata kusikiliza vipindi vya redioni kuhusu ardhi. Nimegundua mambo mengi, hivyo tunaweza kupeleka ajenda zetu kwenye halmashauri ya kijiiji ili zijumuishwe kwenye ajenda nyingine.


Je, ninatakiwa nifanye nini pale ninaponyang'anywa ardhi yangu kimakosa au ninapopoteza umiliki wa ardhi yangu kimakosa?
Unachotakiwa kujua ni mtu au chombo gani ambacho kimechukua ardhi yako, kisha ujue kimeichukua kwa kutumia kigezo gani. Kama ni kwa maamuzi ya mahakama basi unaweza kuyakatia rufaa hayo maamuzi na kama ni kwa njia za ubadhilifu basi unaweza kufungua kesi dhidi ya wahusika.



Hivi unajua ya kuwa yule mwekezaji ambaye ametuma maombi ya kupewa ardhi kubwa kupita kiasi.....hapa kijijini kwetu ni mke wa Kamishna wa Ardhi? Kama tukimyima mke wake ardhi si tutakosa hati miliki za kimila au ardhi yetu kuchukuliwa kabisa.
Tusiwe na wasi wasi. Sheria zinasema kuwa ardhi ya kijiji ipo chini ya baraza la kijiji kama msimamizi kwa manufaa ya wanakijiji wote. Kwa maana hiyo wanakijiji ndiyo tuna mamlaka ya mwisho juu ya ardhi yetu. Kama hana sifa za kupewa ardhi hawezi kupewa kwa sababu ni mke wa kamishna. Kingine kinachotupa nguvu sasa hivi ni hati yetu ya kijiji ambayo ilikabidhiwa kwenye uongozi wa kijiji kuidhinisha ardhi hii yote , sasa tuna mamlaka nayo na maamuzi pia.



mimi na ndugu yangu tunapendana sana, ila hatuelewani kwenye mipaka ya shamba alilotupa baba. Ningependa jambo letu lipate kusuluhishwa bila kwenda mahakamani.
Nakushauri kwenda kwenye baraza la ardhi (baraza la ardhi la kijiji) wao wana mamlaka ya kufanya usuluhishi wa migogoro ya namna hiyo.


Tumesikia faida za hati miliki za kimila lakini hatujui tuanzie wapi kuzipata
Utoaji wa hati miliki za kimila ni zoezi lianalofanywa na kuratibiwa na serikali. Zoezi hili huhusishwa upimaji wa mipaka ya kijiji pamoja na maeneo yanayomilikiwa na wananchi. Wananchi hushirikishwa pindi timu ya wataalamu wa serikali wafanyapo zoezi la upimaji. Wananchi tutapewa taarifa kupitia uongozi wa serikali ya kijiji pindi kijiji chetu kitakapofikiwa na zoezi la upimaji



Mimi na mume wangu ni wachapa kazi, Tumeweza kupata ardhi kubwa sana mpaka ndugu zetu wanatuombea mabaya ili waje kupora ardhi pindi mmoja wetu atakapofariki. Sijui tufanyaje ardhi hii tuliyoitafuta kwa shida iendelee kubaki kwenye familia yetu.
Pole sana..
Mimi na mume wangu tulipata elimu kutoka kwa wasaidizi wa sheria kabla ya kwenda kuandikisha viwanja vyetu kwa ajili ya kupata hati miliki ya kimila. Tuliandikisha majina yetu sote wawili kama wamiliki wa pamoja. Msaidizi wa sheria alituambia kuwa sheria za ardhi zinatambua umiliki wa pamoja ambapo ikitukea mmoja kafariki, mali yote inabaki kwa yule aliyebaki bila mtu mwingine kuingilia. Ni vema pia kama mtaandika wosia ili kuepusha matatizo.


Mimi nilitaka kupeleka jina langu ili niwe mjumbe katika Halmashauri ya kijiji...lakini tayari wanawake waliopeleka maombi wamekwishatimia ile idadi ya watatu kama kawaida tufanyavyo hapa kijijini
Hapana...
Tumezoea kuishi kwa mazoea hayo, lakini inatubidi tubadilike sasa. Wanawake mnajitokeza kwa wingi siku hizi kugombea nafasi za uongozi, pelekeni majina yenu kadri muwezavyo hata kama idadi yenu ikizidi ile ya wanaume ni sawa kabisa.
Ohoo!


Nimesikia ya kuwa ardhi yote ya Tanzania ni mali ya Rais. Je ukitaka kuipata lazima yeye atoe ruhusa ndo upewe? Sijui nitampataje kwa sababu nahitaji ardhi kihalali
Rais ni msimamizi tu wa ardhi kwa niaba ya Watanzania wote kwa kipindi anachokuwa madarakani. Mfano mlinzi anayelinda shamba wakati wa usiku au mchana mpaka mwenzake atakapokuja kumpokea. Chombo chenye mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji ni halmashauri ya kijiji, hivyo peleka maombi yako kwao.


Mwekezaji wa kigeni anaweza kupata ardhi ya kijiji kwa ajili ya uwekezaji?
Anaweza..
Anaweza vipi wakati mtu asiye raia wa kitanzania haruhusiwi kumiliki ardhi ya Tanzania?
Ndiyo, mwekezaji yeyote yule anaweza kupata ardhi ya kijiji kwa ajili ya uwekezaji, Mwekezaji wa kigeni anaweza kupata ardhi ya kijiji kwa ajili ya uwekezaji kupitia Kituo cha uwekezaji Tanzania, kituo hicho kitampatia mwekezaji huyo haki zitokanazo na hiyo ardhi.


Jamani wale wakina mama tunaopenda maendeleo, tujiunge pamoja kama kikundi tutume maombi ili tupewe eneo ambalo litakuwa letu chini ya kikundi chetu cha maendeleo.
Hee!! hiyo hati itakuwa na jina la nani
Kiwanja hicho kitaandikwa kwa jina la kikundi na siyo mtu binafsi


Hizo hati miliki za kimila naziona kama ujanja ujanja wa enzi za wakoloni. Wakoloni walizitumia kuwarubuni na kunyang'anya mashamba mababu zetu. Mbona siku zote tunamiliki mashamba yetu bila ya hizo hati za kupimiwa tena bila matatizo yoyote?
Hati miliki za kimila ni shahada ambayo inathibitisha kimaandishi ya kwamba wewe ndiye mmiliki halali wa eneo husika ambaye unatambulika na serikali ya kijiji. Hii inaongeza ulinzi kwa mmiliki wa ardhi na kwamba mtu mwingine yeyote hawezi kuchukua eneo lako isipokuwa serikali kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria.


Jamani hawa wapimaji wanapima mipaka ya kijiji chetu vibaya, je hatuhitaji kushirikishwa kutoa ufafanuzi.


Ni kweli kabisa unavyosema, ushirikiano ni lazima kutoka pande zote mbili, hii itasaidia kupunguza migogoro hapo baadaye. Na hata sheria ya ardhi ya Vijiji inasema Baraza la Kijiji lazima lishirikishe wanakijiji kwa kupitia mkutano mkuu wa kijiji


Umesikia taarifa zinazosambaa mtaani? Mzee Kishazi anagombea tena nafasi ya uenyekiti wa kijiji aendeleze tabia yake ya kuwanyang'anya wanyonge mashamba yao na kuwapa wenye pesa.


Sikiliza bwana...hawezi kupata kura zetu tumemchoka. Tena ajitafakari mara mbili mbili, kama aliweza kipindi kile, mambo yamebadilika sana siku hizi. Kuna mifumo mbalimbali ya kutuwezesha wananchi kupata haki zetu kama vile mabaraza ya vijiji, hata na wilaya. Pia kuna wasaidizi wa sheria katika vijiji vyetu.


Tumesikia faida za hati miliki za kimila lakini hatujui tuanzie wapi kuzipata


Utoaji wa hati miliki za kimila ni zoezi linalofanywa na kuratibiwa na serikali. Zoezi hili huhusisha upimaji wa mipaka ya kijiji pamoja na maeneo ya watu binafsi.


Hivi ni kwa nini natakiwa kulipia kodi ardhi ambayo ni mali yangu yenye hati miliki kabisa?


Ardhi ni mali ya umma, mtanzania yeyote ni lazima alipie kodi ya ardhi kwa sababu pamoj na kwamba ameinunua au anaimiliki ardhi, yeye anabaki kuwa mpangaji tu wa ile ardhi. Na usipolipa kodi ya ardhi ni kosa la kisheria, utaadhibiwa na hata kunyang'anywa ardhi hiyo.



HEAD OFFICE
Ilala Shariff Shamba, Bungoni Area, Plot No. 31 | Tel: +255 22 2862865
P.O. Box 9460, Dar es Salaam, Tanzania | Website: www.tawla.or.tz
Free legal aid services:
Call toll-free Numbers: 0800110017 / 0800751010